

SHULE YA SEKONDARI MIANGALUA
S. L. P 120,
SUMBAWANGA.
Barua pepe:
miangaluasecondaryschool@gmail.com
Mob: 0767447647
Tarehe: 15/12/2020

Kumb Na. SDC/MGL/JI/2021

Jina la Mwanafunzi
S. L. P
.....

YAH: **KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MIANGALUA WILAYA YA SUMBAWANGA**
MKOA WA RUKWA MWAKA 2021

1.0 Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kijiunga kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021. Shule ya sekondari MIANGALUA ipo umbali wa km 1 kutoka kijiji cha Miangalua kuelekea Tunduma upande wa kulia.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shulenii kuanzia tarehe 10/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 18/01/2021 ndani ya siku saba.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare za Shule

a) Wavulana

1. Mashati mawili meupe ya mikono mifupi
2. Suruali mbili rangi ya blue bahari
3. Viatu vyeusi jozi mbili vya ngozi na vya kufunga na Kamba (visiwe na vizigino virefu)
4. Soksi nyeupe jozi mbili
5. Sweta rangi ya zambarau isiyo na maandishi
6. Raba jozi moja kwa ajili ya michezo
7. Bukta mbili na t-shirt za michezo rangi nyekundu
8. Track moja nyekundu
9. Nguo za kazi suruali mbili za kitambaa rangi ya dark blue, t-shirt mbili rangi ya blue.

NB: Hauruhusiwi kuja na nguo nyingine mbali na uniform zilizopendekezwa na shule

b) Wasichana

1. Blauzi nyeupe mbili mikono mifupi
 2. Sketi za marinda mbili ndefu rangi ya blue bahari
 3. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba jozi mbili (usije na viatu vingine vyenye visigino virefu – high heel)
 4. Soksi nyeupe jozi mbili
 5. Raba jozi moja kwa ajili ya michezo
 6. Sweta rangi ya zambarau isiwe na maandishi
 7. Bukta mbili na t-shirt za michezo rangi nyekundu
 8. Track moja ya blue
 9. Nguo za kazi gauni mbili rangi ya kijani nyingine damu ya mzee
- NB: huruhusiwi kuja na nguo nyingine mbali na uniform zilizopendekezwa na shule.

c) Zangi ya hijab ifanane na sare za shule.

2.2 Michango ya chakula na vifaa vya hostel

1. Mahindi gunia mbili, gunia moja kwa muhula
2. Maharage debe tatu (debe 1 na nusu kwa muhula)
3. Fedha Tsh 60,000/= kwa ajili ya malipo ya mpishi na mahitaji ya jikoni (unaweza kule Tsh 30,000/= kwa muhula)
4. Blanket moja, taulo mbili na mto, shuka mbili za rangi blue bahari au pink
5. Godoro futi 3 upana inch 3
6. Sahani, kikombe na bakuli
7. Matibabu ni jukumu la mzazi/mlezi
8. Uje na kiti na meza vya chuma (vipimo vinapatikana shulenii)

2.3 Mahitaji mengine

1. Jembe moja, fyekeo moja, fagio moja (aina chelewa), ndoo mbili za lita 10 (uje na vifaa siyo fedha)
2. Daftari, kalamu, penseli pamoja na mkebe

3.0 Sheria na kanui muhimu za shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na 25 ya mwaka 1978, na kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu, sayansi na teknolojia yenye dhamana ya elimu chini ya Ofisi ya Rais – Tamisemi yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu.

Unatakiwa kuzinagtia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shulenii.

- a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani nan je ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparations)
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu kuwepo ndan nan je ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii
- f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi, na mazingira ya shule
- g) Kuvala sare ya shule wakati wowote unapotakiwa

- h) Kuzinagatia ratiba ya shule wakati wote
- i) Kutunza mali za umma


3.1 Makosa ya fuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule

- a) Wizi
- b) Uasherati na ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyta kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kuber n.k
- e) Kupigana au kupiga
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- g) Kudharau bendera ya taifa
- h) Kuwa mjamzito/kupata mimba au kusababisha mimba
- i) Kutoa mimba
- j) Kuoa au kuolewa
- k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- l) Kukataa adhabu kwa makusudi
- m) Kuwa na simu ya mkononi

4.0 Mambo mengine ya muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shulen na mwanafunzi

- a) Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.
Form hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakapo ripoti shulen
- b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa yajinai
- c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule
- d) Tafadhali soma kwa umakini maelezo, maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII



.....

GISHI MPYENI MILUNDI
MKUU WA SHULE

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI SHULE YA SEKONDARI MIANGALUA

FOMU YA MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi..... mwanafunzi wa kidato cha katika shule ya sekondari Miangalua. Naahidi kwamba sitashiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai katika kipindi chote nikiwa mwanafunzi hapa shleni. Na endapo nitashiriki katika makosa hayo hapo juu nichukuliwe hatua za kinidhamu ikiwemo kufukuzwa shule.

..... SAHIHI YA MWANAFUNZI

UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI

Mimi nikiwa mzazi/mlezi wa mwanafunzi Nakubaliana na ahadi yake ya kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai na naahidi kumsaidia katika kuitekeleza. Naahidi kumwongoza na kumsimamia.

..... SAHIHI YA MZAZI/MLEZI

NB: Kutoteketeza ahadi hiyo kutasababisha mwanafunzi achukuliwe hatua kali za kinidhamu ikiwemo kufukuzwa shule.

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
SHULE YA SEKONDARI MIANGALUA**

**FOMU YA KUKUBALI/ KUTOKUBALI NAFASI YA KIDATO CHAKATIKA SHULE YA
SEKONDARI MIANGALUA MWAKA.....**

1. Mimi.....kidato cha.....
katika shule ya sekondari Miangalua nimezisoma kwa makini sana sheria za shule na naahidi kuzifuata. Vilevile nimesoma kwa uangalifu sana maagizo ya kujunga na shule na naahidi kuwa nitafika na vitu vyote nilivyoagizwa.

.....
SAHIHI YA MWANAFUNZI

UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI

Mimi nikiwa mzazi / mlezi wa
mwanafunzi..... nakubali na ahadi zake na naahidi
kumsaidia katika kuzitekeleza. Naahidi kumtimizia mahitaji yake yote ya Shule kwa
wakati unaotakiwa.

.....
SAHIHI YA MZAZI/ MLEZI.

(Kutotekeleza maagizo kutasababisha Mwanafunzi akose masomo na mzazi/mlezi kuchukuliwa hatua)

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

SHULE YA SEKONDARI MIANGARUA

FOMU YA KUANDIKISHWA SHULENI NA HABARI ZA MZAZI / MLEZI WA MWANAFUNZI

A: HABARI ZA WANAFUNZI

1. Jina kamili kama ulivoandikishwa kwenye mtihani wa darasa la saba
2. Tarehe ya kuzaliwa
3. Dini
4. Mahali ulipozaliwa.....
5. Shule uliyomaliza darasa la saba.....

B: HABARI ZA MZAZI / MLEZI

1. Jina kamili.....
2. Wewe ni mzazi au mlezi..... !..kama ni mlezi eleza
uhusiano wako na mwanafunzi.....
3. Kazi yako
4. Mahali pa kazi.....
5. Dini
6. Wilaya ya nyumbani
7. Maelezo mafupi kuhusu afya ya mwanafunzi
8. Anuani ya nyumbani
9. Namba ya simu.....

Nina dhibitisha kwamba taarifa zilizotolewa hapo juu ni kamili na kweli.

.....
SAHIHI YA MZAZI / MLEZI.